**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**ILIYOKETI DAR ES SALAAM**

**MAOMBI YA ANUAI NA. 202 YA 2021**

(Maombi ya Anuai yanatokana na uamuzi wa Mahakama hii uliotolewa Tarehe 11 Mei 2021 katika Maombi ya Marejeo Na. 26 ya 2020)

**BAINA YA**

**SEIFI IMPEX LIMITED..................................................MLETA MAOMBI**

**NA**

**ERNEST KIKOTI.........................................................MJIBU MAOMBI**

**UAMUZI MDOGO**

**06/06/2022 & 30/06/2022**

**K. T. R MTEULE, J.**

Mleta Maombi **SEIFI IMPEX LTD.** ameleta maombi haya akiomba kibali cha kufungua shauri nje ya mda ili aweze kufungua shauri la Marejeo kati ya Seifi Impex Limited dhidi ya Ernest Kikoti. Mleta maombi anaiomba Mahakama itoe amri zifuatazo:-

i. Kwamba Mahakama itoe kibali cha nyongeza ya mda ili kufungua shauri la marejeo nje ya mda.

ii. Nafuu nyingine yoyote Mahakama itaona kuwa inafaa na ya haki (just).

Historia fupi ya shauri hili ni kwamba Mjibu Maombi aliajiriwa na Mleta Maombi tarehe 01 Oktoba 2012 katika nafasi ya uwakala kama

Labour Court Tz

Afisa Forodha (clearing and forwarding). Ajira ilikuwa ni ya mkataba wa mwaka mmoja uliokuwa unarudiwa hadi tarehe 23 Oktoba 2015, ambapo aliachishwa kazi kwa utovu wa nidhamu kwa kosa la kutofika kazini (abscondment). Mjibu Maombi hakuridhika na uamuzi wa kuachishwa kazi hivyo kufungua shauri la mgogoro wa kazi mbele ya Tume ya Usuluhishi (Tume). Mjibu Maombi alishinda Tuzo katika Tume ambapo mleta maombi hakuridhika na hivyo kufungua shauri la Marejeo Na. 267 la 2020 katika mahakama hii. Shauri hili lilitupwa (struck out) na Mheshimiwa Jaji Aboud kutokana na matatizo ya kiufundi.

Pamoja na maombi ya faragha, Mleta Maombi aliambatanisha kiapo, ambacho kinaeleza mtiririko mzima wa mgogoro huu uliopelekea maombi haya kama ilivyoelezwa hapo juu, ambapo Mleta Maombi ameeleza ya kwamba kutokana na ugonjwa alishindwa kufika Mahakamani tarehe 11 Mei 2021, hivyo shauri la Marejeo Na. 267 la 2020 kuendelea upande mmoja na kuondolewa kwa makosa ya kiufundi. Imeelezwa Zaidi katika kiapo kwamba baada ya maombi ya awali kutupwa, mleta maombi bado ana nia ya kuendelea kufungua maombi ya marejeo laikini akawa amepitwa na muda na hivyo kuleta maombi haya kuomba ongezeko la muda.

labourCourt.TZ

Maombi haya yalipingwa na Mjibu Maombi Kupitia kiapo kinzani kilichoapwa na Methuselah Boaz Mafwele, Wakili wa Mjibu Maombi.

Shauri hili lilisikilizwa kwa njia ya maandishi ambapo, Mleta Maombi aliwakilishwa na Bi. Victoria Mgonja, Wakili, na Mjibu Maombi aliwakilishwa na Bw. Methuselah Mafwele, Wakili.

Akifanya mawasilisho kwa niaba ya Mleta Maombi Bi. Mgonja alirudia maelezo aliyotoa katika kiapo na kuongeza kuwa kwa vile maombi ya marejeo hayakusikilizwa kwa msingi wake, anaomba aongezewe muda ili haki ya msingi iweze kutendeka.

Kwa upande wa wasilisho la Mjibu Maombi, yeye alieleza ya kwamba ni matakwa ya kisheria ya kwamba anayeomba kuongezewa mda ni lazima awe na sababu za msingi zilizomfanya achelewe kuleta maombi na maelezo hayo yawe kwenye kiapo. Alieleza kwamba Mleta Maombi amechelewa kwa mda wa mwezi mmoja kwani shauri la Marejeo Na. 267 la 2020 liliondolewa tarehe 11 Mei 2021 na maombi haya yamefunguliwa tarehe 11 Juni 2021. Kuipa nguvu hoja yake alirejea kesi ya John **Sebastiana Cosmas na Wengineo v. Consolidated Tourist & Hotels Investment Limited,** Marejeo Na. 15 ya 2020, Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, iliyoketi Musoma, (Haijaripotiwa).

Baada ya kupitia viapo vya waleta maombi na mawasilisho ya pande zote mbili, Mahakama inaona hoja bishaniwa ni **"je kuna sababu ya msingi ambayo imetolewa na Mleta Maombi ili Mahakama iyakubali maombi ya kufungua shauli la Marejeo nje ya mda?".**

Katika kujibu hoja bishaniwa, Bi. Mgonja ameeleza kwenye kiapo chake ya kwamba sababu ya kuchelewa kufungua maombi ya marejeo ni ugonjwa na hivyo tarehe 11 Mei 2020 ambapo Shauri la Marejeo Na 267 la 2020 lilipangwa kusikilizwa pingamizi la awali liliondolewa. Katika kiapo chake aliambatanisha kivuli cha hati ya matibabu ambacho ni Kiambata 1.

Kwa upande wa Mjibu Maombi alieleza Mleta Maombi amechelewa kwa mda wa mwezi mmoja bila kuchukua hatua yoyote kwani shauri la Marejeo Na. 267 la 2020 liliondolewa tarehe 11 Mei 2021 na maombi haya yamefunguliwa tarehe 11 Juni 2021.

Katika utatuzi wa hoja hii Kanuni ya 56(1) ya Kanuni za Mahakama za Kazi, 2007 inahusika. Kanuni inaeleza:-

> *56 (1) "The court may extend or abridge any period prescribed by these rules on application and on good cause shown, unless the court is precluded from doing so by any written law."*

LabourCourt.tz

Kutokana na kifungu tajwa, mahakama hii ina mamlaka ya kisheria kuongeza mda wowote chini ya Kanuni hii ikiwa Mwombaji/Waombaji wametoa sababu ya msingi ya uchelewaji. Mwobaji katika shauri hili aliiomba Mahakama nyongeza ya mda kwa sababu alikuwa anaumwa. Kwa kuanza na hoja ya ugonjwa, ushahidi wa taariza za kitabibu uliombatishwa na kiapo kama Kiambata Na.1 zinaonyesha mwombaji alihudhuria matibabu tarehe 10 Mei 2021 na kuwa na kibali cha kutofanya kazi kwa mda wa siku tatu (03).

Mahakama hii inatambua ya kwamba ugonjwa ni moja ya sababu inayoweza kuwa kigezo cha Mahakama kutoa nyongeza ya mda lakini sababu lazima ithibitishwe. Mahakama hii katika kesi ya **Fredrick Mdimu dhidi ya Cultural Heritage Ltd.,** Marejeo Na. 19 of 2011, Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, iliyoketi Dar es Salaam, ilieleza ya kwamba:-

> *"Ugonjwa ni Sababu inayokubalika katika kuchelewa kufungua shauri ndani ya mda. Lakini sababu hii lazima ithibitishwe na kisiwe kisingizio. Kama mwombaji alikuwa anatabiwa hospitali ni kwanini hakutoa hati ya taarifa ya matibabu ili kuunga mkono hoja hiyo?"*

Haina ubishi kwamba wakili wa mleta maombi aliugua na ushahidi umetolewa.

Ni wazi kibali cha wakili wa mleta maombi kutofanya kazi kilikuwa kinakoma 13 Mei 2021. Katika kiapo chake mleta maombi ameeleza pia kuwa hakuwa na taarifa za amri ya mahakama kufutilia mbali maombi hayo ya marejeo hadi tarehe **3 Juni** alipokuja mahakamani kuhudhuria kesi nyingine mbele ya Mhe. Jaji Muruke ndipo alipopewa taarifa na karani wa Mahakama kuwa shauri lilifutiliwa mabali.

Katika Kesi ya **Daudi Hag a v. Jenitha Abdan Machanju,** Madai ya Masahisho No. 19 of 2006, Mahakama ya Rufani ya Tanzania, iliyoketi Tabora (Haijaripotiwa), ambapo ilielezwa ya kwamba:-

> *"Mtu yeyote anayeomba nyongeza ya muda anatakiwa aileze Mahakama alichokuwa akifanya kila siku ya uchelewaji ili kuiwezesha Mahakama kutumia mamlaka yake."*

Hata hivyo ni msimamo wa kisheria pia idadi ya siku za kuchelewa zisiwe nyingi kupita kiasi. (Angalia. **Lyamuya Construction Company Ltd vs. Board of Registered Trustees of Young Women's Christian Association of Tanzania,** Civil Application No. 2 of 2010, the Court of Appeal of Tanzania, at Dar es Salaam, (Unreported). Kwa vile mleta maombi hakuwepo wakati maombi yake



LabourCourtTz

yalipotupiliwa mbali hadi tarehe 3 Juni 2020 muda usiokuwa na maelezo unaanza kuhesabiwa tarehe 3 Juni alipopata taarifa hadi tarehe 11 Juni alipofungua maombi haya ya kuomba ongezeko la muda. Kuna idadi ya siku 8 ambzo hazijatolewa maelezo.

Kutokana na msimamo wa kisheria ni wazi uchelewaji wa siku 8 si mkubwa kupita kiasi. Katika hali ya kawaida hiki kinaweza kuwa ni kipindi ambacho maombi haya yalienda kuandaliwa na kuwasilishwa Mahakamani.

Kwa mazingira haya na ili haki ya msingi iweze kufikiwa, Mahakama inatumia mamlaka ya chini ya Kanuni ya 56 (1) ya Kanuni za Mahakama ya Kazi, Tangazo la Serikali Na. 106 la 2007 kuongeza muda wa mleta maombi kufungua maombi ya marejeo nje ya muda. Maombi hayo yawasilishwe mahakamani ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya hukumu hii.

Amri hii imetolewa Dar es salaam leo tarehe 30 Juni, 2022.

Labour Court TZ

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA (The High Court of Tanzania) (Labour Division) DIVISHENI YA MAHAKAMA YA KAZI

**KATARINA REVOCATI MTEULE**

**JAJI**

**30/06/2022**